

Kujiandikisha kupiga kura

Unaweza kujiandikisha kupiga kura katika jimbo la Michigan ikiwa:

- Wewe ni raia wa Marekani
- Mkazi wa Michigan kwa angalau siku 30
- Wenye umri wa miaka 17.5 na 18 Siku ya Uchaguzi watapiga kura (wenye umri wa miaka 16 na 17 wanaostahiki wanaweza kujiandikisha mapema kupiga kura)
- Hutumikii kifungo jela au gerezani kwa sasa

Jiandikishe mtandaoni kwenye Michigan.gov/Vote au chapisha fomu ya kujiandikisha iliyotafsiriwa iliyopo kwenye Michigan.gov/SOSLanguageForms.

Piga kura vile upendavyo: Machagu yako ya kupiga kura katika jimbo la Michigan

- **Piga kura kwa njia ya barua:** Omba karatasi ya kura ya mtu asiyekuwepo itumwe nyumbani kwako ili upige kura kwa urahisi na kwa hali inayofaa. Omba karatasi ya kura ya mtu asiyekuwepo kwa njia ya mtandao kupitia Michigan.gov/Vote au pakua maombi yaliyotafsiriwa kupitia Michigan.gov/SOSLanguageForms.
- **Piga kura mapema ana kwa ana:** Tembelea mapema kituo cha kupigia kura kilicho karibu nawe ili kupiga kura mapema na ana kwa ana. Upigaji kura wa awali kwa ajili ya Novemba unanza jimbo zima Oktoba 26 hadi Novemba 3.
- **Piga kura Siku ya Uchaguzi:** Tembelea eneo la kupigia kura lililo karibu nawe ili kupiga kura Siku ya Uchaguzi.
- **Ukalimani katika vituo vya kupigia kura:** Una haki ya kuja na mkalimani atakayekusaidia wakati wa kupiga kura. Mkalimani wako hawezi kuathiri kura yako, awe mwajiri wako, wakala wa mwajiri wako, au afisa au wakala wa chama chako cha wafanyakazi.
- **Huhitaji Utambulisho wa picha:** Iwapo huna kitambulisho chenye picha, bado unaweza kupiga picha.
- **Raia wanaorejea:** Katika jimbo la Michigan watu ambao hapo awali walikuwa na hatia/walifungwa bado wanastahili kujiandikisha na kupiga kura, hata kama wapo kwenye kifungo cha nje au uangalizi.

Haki zako za kupiga kura katika jimbo la Michigan

Ulinzi wa uchaguzi na vitisho kwa mpiga kura

Iwapo utakabiliwa na matatizo yoyote ya kupiga kura Siku ya Uchaguzi au kabla, au ikiwa una maswali kuhusu upigaji kura, piga Simu ya Msaada wa Ulinzi wa Uchaguzi kwa msaada:

- 866-OUR-VOTE (866-687-8683)

Pata maelezo zaidi kuhusu kupiga kura katika jimbo la Michigan kwa Kiswahili kwenye Mi.gov/SOSLanguage au changanua msimbo QR.

